

KUKITHIRI KWA MAKOSA YALIYOZOELEKA KATIKA MATUMIZI YA KISWAHILI SANIFU: UCHUNGUZI WA MAKOSA MAALUMU

Issaya Lupogo
Chuo Kikuu Mzumbe – Tanzania
islupogo@mzumbe.ac.tz

Ikisiri

Kumekuwa na mazoea ya kufanya makosa¹ katika matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu. Licha ya kukithiri kwa makosa hayo, hakujawa na wakemeaji au wakosoaji wengi kama ilivyo katika lugha ya Kiingereza, ambapo yejote anayekosea lugha hiyo, hukosolewa vikali. Makala hii ni matokeo ya ushuhudiaji kwa njia ya kusikiliza na kusoma habari mbalimbali rasmi kama vile ripoti na/au taarifa mbalimbali zinazotolewa na taasisi mbalimbali, vitabu vilivyochapishwa, matangazo katika taasisi na asasi mbalimbali, kurasa za mitandao ya kijamii za vyombo vya habari, na taarifa mbalimbali katika televisheni na radio. Vilevile, mwandishi alishuhudia makosa mengine katika makongamano na mikutano ya kitaaluma aliyowahi kuhudhuria. Majina ya vyanzo vilivyobainika kufanya makosa hayo hayajawekwa bayana kwa sababu za kitikeli. Makala hii imemakinika kategoria kadhaa tu za makosa: makosa ya kuunganisha na kutenganisha maneno, makosa ya kuchangaya herufi, na kudondosha na kuchopeka sauti/herufi “h” kimakosa. Makala hii imebaini kwamba yapo makosa ambayo yamekithiri kiasi cha kuonekana kama yameshalalishwa. Makala inatoa mapendekezo kadhaa ya kurekebisha hali hii ya utitiri wa makosa yaliyozoeleka katika matumizi ya Kiswahili sanifu: kuendeshwa kwa semina za namna ya kuepuka makosa hayo kwa watu mashuhuri/maarufu na wanahabari; vyombo vyenye mamlaka ya kusimamia Kiswahili viunde mikakati ya kutafuta suluhihisho la tatizo hilo; wanaokosea kwa sababu ya athari za lugha mama wanatakiwa kuwa na utambuzi wa tatizo hilo na kujitahidi kulidhibiti; wataalamu wa Kiswahili na Waswahili wenye mapenzi mema na lugha yao wasimame kidete kuwarekebisha na kuwakosoa wanaobananga Kiswahili sanifu.

¹ Katika makala hii dhana ya ‘makosa’ inajumuisha pia dhana ya ‘dosari’.

2 ISSAYA LUPOGO - KUKITHIRI KWA MAKOSA YALIYOZOELEKA KATIKA
MATUMIZI YA KISWAHILI SANIFU

1.0 Utangulizi

Ifahamike kwamba mwandishi wa makala hii anafahamu ni vigumu sana kuwa na waraka mrefu ambao hauna kosa lolote. Huenda hata katika makala hii, kuna makosa kadhaa. Makosa haya yanaweza kutazamwa kwa namna kuu mbili. Kwanza, ni makosa ambayo hutokana na kukosea kuandika neno ambalo si sahihi kwa bahati mbaya, kwa maana ya kwamba unajua vema neno sahihi lakini umekosea kuliandika bila wewe mwenyewe kujua. Kwa maoni yangu, makosa haya hayana shida kubwa, na endapo mwandishi wa waraka au ujumbe akipitia tena vema alichokiandika, ana uwezo wa kurekebisha kosa husika. Pili, ni makosa ambayo mwandishi hajui kama ni makosa, yaani yeze anajua kwamba alichokiandika ni sahihi ilihali amekosea. Haya ndiyo makosa mabaya sana, na ndiyo yanayojadiliwa katika makala hii. Hii ni kutokana na sababu kwamba mwandishi wa waraka au ujumbe aliyefanya aina hii ya makosa, hata akirudia kupitia ujumbe wake mara nyingi, hawezikubaini kosa lolote. Pia, mtu huyo asiporekebishwa, ataendelea kufanya makosa hayo kila anapoandika au kuongea.

Wanaisimu wanakiri kwamba si jambo rahisi kutofautisha dhana ya makosa na dosari². Sababu ya ugumu wa kutofautisha dhana hizi ni kutokana na mwingiliano uliopo baina yake. Feltsen (2009) anabainisha kwamba kosa linahusisha mtumiaji wa lugha kuvunja kanuni za lugha kutokana na kushindwa kutumia ipasavyo ujuzi wa lugha alionao. Ina maana kwamba mtumiaji huyu wa lugha anakosa umahiri wa kutumia lugha yake. Wakati dosari inafafanuliwa kwamba ni matokeo ya kutokuwa na ujuzi wa lugha katika eneo fulani ambalo mtu anavunja sheria au kanuni katika lugha. Kwa hiyo, mtu anayefanya kosa ni rahisi kujirekebisha kwa sababu anajua wapi alipokosea wakati mtu anayefanya dosari hawezikujirekebisha hadi pale atakapoelekezwa.

Kamusi ya Kiswahili Sanifu ya TUKI (2014) inafafanua makosa kuwa ni hali ya kwenda kinyume na kanuni fulani na dosari ni hali inayopunguza ukamilifu wa kitu. Ukichunguza tofauti za maana ya makosa na dosari, utabaini kwamba mstari unaozitenganisha dhana hizi ni mdogo sana. Kwa hiyo, makala hii inatumia neno ‘makosa’ kama dhana kuu inayowakilisha dosari pia. Kwa mantiki hiyo, makala hii inashughulikia masuala yote mawili, makosa na dosari.

Kiswahili sanifu kimetokana na kusanifishwa kwa lahaja ya Kiunguja baada ya lahaja ya Kimvita iliyokuwa ikikaribiana nayo kiushindani

² Dhana hizi kwa lugha ya Kiingereza zinajulikana kama *mistakes* na *errors* mtawalia.

kuachwa (Whiteley, 1974). Hili linaoneshwa pia na Kiango (2002) na Hans (2014) wanaobainisha kwamba kipindi cha ukoloni paliibuka mjadala mionganoni mwa watawala juu ya lugha ipi itumike ukanda wa Afrika Mashariki (Kenya, Uganda na Tanzania) katika sekta zote rasmi, na ndipo Kiunguja kikachaguliwa mionganoni mwa lahaja nyingi zilizokuwapo. Lahaja hiyo ilisanifishwa baadaye na kuwa Kiswahili sanifu. Maganga (1991) anabainisha Kiswahili sanifu kuwa ni lugha rasmi itumikayo katika kazi za chama na serikali, katika masuala ya uchapishaji wa maandiko ya kitaaluma, na katika vyombo vyatuhari. Maana ya Kiswahili sanifu ya Maganga ndiyo iliyyotumika katika makala hii.

Makosa yaliyozoleka katika matumizi ya Kiswahili sanifu ni jumla ya ubanangaji na ukengeukaji wa namna yoyote unaofanywa na watumiaji wa lugha ya Kiswahili sanifu kwa ujumla. Makosa hayo husababishwa na watu kutozingatia kanuni za Kiswahili sanifu. Kutozingatia huko husababishwa na mtu kutojihusisha kufuatilia kujua kanuni hizo, kwa kutojua au wakati mwingine kwa kupotoshwa na watu wengine hususani wanahabari au watu maarufu kwa sababu wao ndio husikilizwa sana na watu wengi. Aidha, wengine hukosea kwa kupuuuzia na kutokuwa makini ilhali wanajua kanuni za Kiswahili sanifu. Kwa hiyo, makala hii inalenga kubainisha makosa mbalimbali na kuyarekebisha.

Makala hii ni matokeo ya ushuhudiaji kwa njia ya kusikiliza na kusoma habari mbalimbali rasmi kama vile ripoti na/au taarifa mbalimbali zinazotolewa na taasisi mbalimbali, vitabu vilivyochapishwa, matangazo katika taasisi na asasi mbalimbali, kurasa za mitandao ya kijamii za vyombo vyatuhari, na taarifa mbalimbali katika televisheni na redio. Vilevile, mwandishi alishuhudia makosa mengine katika makongamano na mikutano ya kitaaluma aliyowahi kuhudhuria. Majina ya vyanzo vilivyobainika kufanya makosa hayo hayajawekwa bayana kwa sababu za kiitikeli.

2.0 Kategoria za Makosa Yaliyozolekea katika Kiswahili Sanifu

Yapo baadhi ya makosa yanayoonekana kushika kasi kiasi cha kuonekana kama yamehalalishwa. Kwa mfano, makosa yafuatayo yametamalaki katika miktadha mingi ya matumizi ya Kiswahili sanifu, kama vile katika matangazo kwenye taasisi mbalimbali, taarifa katika vyombo vyatuhari, na nyaraka mbalimbali za taasisi:

“*Nakadhalika*” badala ya “na kadhalika”
“*Dhalura*” badala ya “dharura”
“*Tahadhali*” badala ya “tahadhari”

4 ISSAYA LUPOGO - KUKITHIRI KWA MAKOSA YALIYOZOELEKA KATIKA MATUMIZI YA KISWAHILI SANIFU

“*Tafadhari*” badala ya “tafadhalii”
“*Maazimisho*” badala ya “maadhimisho”
“*Baadae*” badala ya “baadaye”
“*Kwasababu*” badala ya “kwa sababu”
“*Kwaajili*” badala ya “kwa ajili”
“*Kuwakilisha hoja*” badala ya “kuwasilisha hoja”
“*Fezeha*” badala ya “fedheha”
“*Taraka*” badala ya “talaka”
“*Luga*” badala ya “lughaa”
“*Auna*” badala ya “hauna”
“*Asiye fika*” badala ya “asiyefika”
“*Anamo ishi*” badala ya “anamoishi”
“*Hairisha*” badala ya “ahirisha”

Kifuatacho ni Kielelezo kinachoonesha makosa yaliyozoeleka katika matumizi ya Kiswahili:

Michezo - Ligi ya England kuendelea Kesho

Mechi kati ya Arsenal na West Ham imehairishwa kutokana na uwezekano wa kuwepo kwa mgomo wa madereva wa treni.

Corona yazuia Watanzania DRC - .

2 days ago · ... ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) imehairishwa kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa homa ya virusi vya corona.

Kama ikitokea mechii yoyote kwenye chaguzi zako imehairishwa au haijachezwa kama ilivyotakiwa na kukuacha wewe kwenye tiketi ...



Kielelezo 1: Mfano wa Kosa Lililozoeleka “imehairishwa” kutoka baadhi ya Vyanzo vya Kuaminika vya Habari

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Kielelezo 1 kinaonesha vyombo nya habari vitatu³ tofauti vilivyokosea kuandika neno “imeahirishwa”, badala yake, vyombo hivyo vyote vimeandika “imehairishwa”.

Licha ya makosa hayo kutamalaki kwa kiasi kikubwa, bado hakuna andiko madhubuti linaloeleza makosa hayo na kuwakumbusha watumiaji wa Kiswahili sanifu hususani wale wanaotumia lugha hiyo katika miktadha rasmi kuyaepuka makosa hayo au kujirekebisha. BAKITA⁴ (2002) liinabainisha baadhi ya makosa na kutoa miongozo mbalimbali ya Kiswahili sanifu. Hata hivyo, kitabu hicho cha BAKITA hakijabainisha makosa mengi yanayofanywa na watumiaji wa Kiswahili sanifu, pengo la maarifa linalofanyiwa kazi na makala hii.

Wakati mwingine mamlaka zinazosimamia lugha ya Kiswahili kama vile BAKITA na BAKIZA⁵ zimekuwa zikilazimika kusanifisha msamiati ambao umetamalaki kimatumizi kimakosa kwa sababu msamiati huo umeshashika hatamu kimatumizi. Mfano wa msamiati huo ni “onyesha”. Neno “onyesha” lenye maana yake ya msingi kuonya kama ambavyo mzizi wake upo bayana kabisa limekuwa likitumika kimakosa kwa muda mrefu badala ya neno mwafaka ambalo ni “onesha”; lenye dhana ya “kuona”. Kwa hivyo, hali ya watu kukosea Kiswahili sanifu ikifumbiwa macho, Kiswahili kitaharibiwa na hatimaye vyombo vyenye mamlaka ya kusimamia lugha ya Kiswahili vitafanya kazi ya kurekebisha na kubadilisha msamiati ulioundwa au kuwekwa ukiwa na mantiki kiisimu na kufuata muundo wa wazungumzaji unaokiuka kanuni za Kiswahili sanifu. Ili kukabiliana na suala hilo, makala hii inaangazia baadhi ya kategoria za makosa yaliyozoleka katika Kiswahili sanifu.

Baada ya kumakinikia matumizi ya Kiswahili sanifu katika miktadha mbalimbali, imekuja kubainika kwamba kuna makosa ambayo yanaweza kuwekwa katika kategoria mbalimbali. Ifahamike kwamba kwa kuwa makosa hayo yako mengi na kila siku yanaendelea kujitokeza mapya, kategoria zilizobainishwa hapa zinaweza kuwa si kategoria pekee ambazo zimeonesha aina zote za makosa. Jedwali la 1 linaonesha baadhi ya kategoria za makosa hayo.

Majina ya vyombo nya habari yameondolewa kwa sababu za kiitikeli.

⁴ BAKITA ni akronimu, kirefu chake ni Baraza la Kiswahili la Taifa

⁵ Hii ni akronimu, kirefu chake ni Baraza la Kiswahili la Zanzibar

**6 ISSAYA LUPOGO - KUKITHIRI KWA MAKOSA YALIYOZOELEKA KATIKA
MATUMIZI YA KISWAHILI SANIFU**

**Jedwali la 1: Baadhi ya Kategoria za Makosa Yaliyozoleka katika
Kiswahili Sanifu na Mifano yake**

Na.	Kategoria za Makosa Yaliyozoleka	Mfano
1.	Makosa ya kimsamiati	-“misamiati” badala ya “msamiati” -“jumbe” nyingi badala ya “ujumbe” mwingi
2.	Kuunganisha maneno kimakosa	-“kwaajili” badala ya “kwa ajili” -“kwasababu” badala ya “kwa sababu”
4.	Kutenganisha maneno kimakosa	-“asiye fika” badala ya “asiyefika” -“anapo ishi” badala ya “anapoishi”
5.	Makosa ya kiurari	-matumizi ya neno “onesha” na “onyesha” katika waraka mmoja badala ya kuchagua neno moja tu -matumizi ya “makala haya” na “makala hii” katika waraka mmoja badala ya kuchagua kirai kimojawapo tu -matumizi ya neno “anuani” na “anwani” katika waraka mmoja badala ya kuchagua neno moja tu
6.	Makosa ya kiuakifishaji	-“Kahigi, 2020, anabainisha kwamba...” badala ya “Kahigi (2020) anabainisha kwamba..”
7.	Makosa ya kuchanganya herufi/sauti (r/l, z/dh, s/th, g/gh)	-“zambi” badala ya “dhambi” -“luga” badala ya “lugha”
8.	Kudondosha na kuchopeka herufi “h” kimakosa	-“eshima” badala ya “hushima” -“haya” badala ya “aya”
9.	Makosa ya upatanisho wa kisarufi	-“nyimbo inapigwa” badala ya “nyimbo zinapigwa”
10.	Makosa katika kujenga umoja na wingi	-“mashule mengi” badala ya “shule nyingi” -“maofisi mengi” badala ya “ofisi nyingi”
11.	Ukanganyaji wa irabu na viyeyushi	-“hatimae” badala ya “hatimaye” -“baadae” badala ya “baadaye” -“kua ⁶ ” badala ya “kuwa” (na kinyume chake)

⁶ Neno linalorejelewa hapa ni kitenzi ambacho mara nyingi hujitokeza kama kitenzi kishirkishi (Yeye alikuwa mwalimu) au kitenzi kisaidizi (Yeye alikuwa anaimba). Inajulikana kwamba neno “kua” pia lina maana ya kuongezeka kwa umri au ukubwa; hii si dhana inayorejelewa katika mfano huu wa kosa lililozoleka

12.	Makosa ya kiakronimu	-“ <i>Chadema</i> ” badala ya “CHADEMA” -“ <i>slp</i> ” badala ya “S.L.P.”
13.	Makosa ya kimuktadha	-“ <i>wasilisha</i> ” badala ya “wakilisha” (na kinyume chake)
14	Kosa la kupishanisha sauti	“- <i>imehairishwa</i> ” badala ya “ <i>imeahirishwa</i> ” “- <i>lasirimali</i> ” badala ya “ <i>rasilimali</i> ”
15	Makosa ya kimantiki	“ <i>nilimkuta hayupo</i> ” badala ya “ <i>sikumkuta</i> ”

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Hizi ni baadhi tu ya kategoria za makosa yaliyozoeleka katika Kiswahili sanifu pamoja na mifano yake michache sana. Ufafanuzi wa makosa yote unafaa kuelezweta katika andiko kubwa; kiwango cha andiko hili (makala), yafaa kujadili sehemu ndogo ya makosa hayo. Hivyo, makala hii inamakinikia kiundani kategoria tatu tu: makosa ya kuchangaya herufi/sauti, makosa ya kuunganisha na kutenganisha maneno; na kudondosha na kuchopeka herufi *h* kimakosa.

2.1 Makosa ya Kuchanganya Herufi/Sauti

Haya ni makosa yanayohusisha baadhi ya watu kuchanganya sauti wanapoandika au kuzungumza. Makosa haya yanagawanyika kulingana na sauti zinazochanganya kama ifuatavyo:

- Makosa ya kuchanganya sauti *g* na *gh*
- Makosa ya kuchanganya sauti *r* na *l*
- Makosa ya kuchanganya sauti *z* na *dh*
- Makosa ya kuchanganya sauti *s* na *th*

2.1.1 Makosa ya Kuchanganya Sauti /g/ na /gh/

Kutoka uwandani, ilibainika kwamba baadhi ya watu hutamka silabi *ga*, *ge*, *gi*, *go*, *gu* badala ya *gha*, *ghe*, *ghi*, *gho*, *ghu* katika maneno na tungo mbalimbali kama inavyojidhihirisha katika mifano ifuatayo:

"gali" badala ya "ghali"
 "garama" badala ya "gharama"
 "sauti guna" badala ya "sauti ghuna"
 "gala" badala "ghala"
 "gasia" badala ya "ghasia"
 "garika" badala ya "gharika"
 "gafla" badala ya "ghafla"
 "gani shairi" badala ya "ghani shairi"
 "gushi cheti" badala ya "ghushi cheti"

8 ISSAYA LUPOGO - KUKITHIRI KWA MAKOSA YALIYOZOELEKA KATIKA MATUMIZI YA KISWAHILI SANIFU

“*faraga*” badala ya “faragha”
“*gafilika*” badala ya “ghafilika”
“*gadhabu*” badala ya “ghadhabu”
“*gorofa*” badala ya “ghorofa”

Kwa kuitia na kusikiliza uwasilishaji wa makala na taarifa mbalimbali za kitaaluma katika makongamano na mikutano ya wanataaluma hususani ya Kiswahili, imebainika kwamba watu kutoka Tanzania Bara wanafanya sana kosa hili ukilinganisha na watu kutoka Zanzibar (Tanzania Visiwani). Huenda sababu mojawapo ni kwamba Zanzibar ndiyo chimbuko la lahaja ya Kiswahili iliyosanifishwa na kupata Kiswahili sanifu kinachotumika hii leo; ambayo ni lahaja ya Kiunguja.

Hii pia ni kategoria ya makosa ambayo haijitokezi upande wa pili wake au kinyume chake. Hii ina maana kwamba haijawahi kubainika kinagaubaga watu wakisema au kuandika mathalani kama ifuatavyo:

“*ghari*” badala ya “gari”
“*gholi*” badala ya “goli”
“*aghizo*” badala ya “agizo” n.k.

2.1.2 Makosa ya Kuchanganya Sauti /r/ na /l/

Haya ni makosa yanayohusisha kuchanganya sauti /r/ na /l/; yaani badala ya kutamka au kuandika sauti /r/ inaandikwa /l/ na kinyume chake.

Mfano A: / r/ badala ya /l/
“*tafadhari*” badala ya “tafadhalii”
“*ghari*” badala ya “ghali”
“*pirika*” badala ya “pilika”
“*mahari* (sehemu)” badala ya “mahali”
“*kura* (chakula)” badala ya “kula”
“*uterezi*” badala ya “utelezi”
“*marezi*” badala ya “malezi”
“*pereka*” badala ya “peleka”
“*mpore*” badala ya “mpole”
“*firimbi*” badala ya “filimbi”
“*firisika*” badala ya “filisika”
“*firamu*” badala ya “filamu”
“*randana*” badala ya “landana”
“*ramba*” badala ya “lamba”

Mfano B: /l/ badala ya /r/

“*anaona fahali*” badala ya “anaona fahari”
“*bebelu*” badala ya “beberu”

"*mahali* (posa)" badala ya "mahari"
"*balabala*" badala ya "barabara"
"*ghaili*" badala ya "ghairi"
"*nulu*" badala ya "nuru"
"*piga kula*" badala ya "piga kura"

Kwa kiasi kikubwa, makosa haya hujitokeza zaidi wakati wa mazungumzo kuliko katika maandishi. Pamoja na sababu ya jumla ya watu kukosa umakini wa kuzingatia kanuni za Kiswahili sanifu, sababu nyingine mahususi katika kategoria hii ni athari ya lugha mama ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili. Mathalani, Wasukuma hutumia sana sauti /r/ kuliko /l/ katika lugha yao. Hivyo, hujikuta wakihawilisha utamkaji huo wanapotumia Kiswahili sanifu.

2.1.3 Makosa ya Kuchanganya Sauti /z/ na /ð/ (dh)

Haya ni makosa ya baadhi ya watu kutumia silabi *za*, *ze*, *zi*, *zo*, *zu* badala ya *dha*, *dhe*, *dhi*, *dho*, *dhu*. Mifano:

"*zambi*" badala ya "dhambi"
"*zuluma*" badala ya "dhuluma"
"*zarau*" badala ya "dharau"
"*zoruba*" badala ya "dhoruba"
"*azabu*" badala ya "adhabu"
"*ghazabu*" badala ya "ghadhabu"
"*bizaa*" badala ya "bidhaa"
"*vitu kazaa*" badala ya "vitu kadhaa"
"*oroza*" badala ya "orodha"
"*wazifa/nyazifa*" badala ya "wadhifa/nyadhifa"
"*zoofika*" badala ya "dhoofika"
"*Tanzania zidi* ya Senegali" badala ya "Tanzania dhidi ya Senegali"
"*zihirika*" badala ya "dhihirika"
"*baada ya ziki faraja*" badala ya "baada ya dhiki faraja"
"*zati*" badala ya "dhati"
"*zihaka*" badala ya "dhihaka"
"*nazifu*" badala ya "nadhibu"

Hii pia ni kategoria ya makosa ambayo haijitokezi upande wa pili wake au kinyume chake. Hii ina maana kwamba haijawahi kubainika kinagaubaga watu wakisema au kuandika kama ifuatavyo:

"*dhaa*" badala ya "zaa"
"*dheeka*" badala ya "zeeka"
"*dhorota*" badala ya "zorota"

10 ISSAYA LUPOGO - KUKITHIRI KWA MAKOSA YALIYOZOZELEKA KATIKA MATUMIZI YA KISWAHILI SANIFU

“*mdhadhi*” badala ya “*mzazi*”

2.1.4 Makosa ya Kuchanganya Sauti /s/ na /θ/ (th)

Imebainika kwamba kuna baadhi ya watu hutamka na/ au huandika silabi *sa, se, si, so, su* badala ya *tha, the, thi, tho, thu* mtawalia.

Mifano:

“*samani ya pesa*” badala ya “*thamani ya pesa*”
“*selasini*” badala ya “*thelathini*”
“*semanini*” badala ya “*themanini*”
“*sibitisha*” badala ya “*thibitisha*”
“*seluji*” badala ya “*theluji*”
“*subutu*” badala ya “*thubutu*”
“*selusi*” badala ya “*theluthi*”
“*sabiti*” badala ya “*thabiti*”
“*samini*” badala ya “*thamini*”

Hii pia ni kategoria ya makosa ambayo hajitokezi upande wa pili wake au kinyume chake. Hii ina maana kwamba hajjawahi kubainika kinagaubaga watu wakisema au kuandika mathalani ifuatavyo:

“*thatha*” badala ya “*sasa*”
“*potha*” badala ya “*posa*”
“*kotha*” badala ya “*kosa*”

Watu walibainika kutumia sauti /th/ badala ya /s/ ni wale wenye matatizo ya kimatamshi yajulikanayo kama kithembe. Hawa ni watu ambao tangu wazaliwe hawawezi kutamka silabi *sa, se, si, so, su*; badala yake hutamka *tha, the, thi, tho, thu*.

Wakati mwingine makosa haya ya kuchangaya sauti au herufi yanababisha kupotosha maana ya neno kabisa. Yapo maneno mengine, ukibadili herufi moja na kuweka nyingine, maana ya neno hilo hubadilika. Mfano wa maneno hayo ni:

- *mahari* na *mahaļi*
- *dhiki* na *ziki*
- *ajaļi* na *ajari*
- *kula* na *kura*
- *kazaa* na *kadħaa*

2.2 Kuunganisha na Kutenganisha Maneno Kimakosa

Kama inavyojibainisha katika anwani, hizi ni aina mbili za makosa zinazoelezwa kwa undani sehemu zifuatazo.

2.2.1 Kuunganisha Maneno Mawili na Kuyafanya kuwa Neno Moja

Hili ni kosa ambalo linahusisha kuunganisha maneno mawili yanayostahili kutenganishwa.

Mfano:

- "vyakutosh" badala ya "vya kutosha"
- "wamwiso" badala ya "wa mwisho"
- "kwasababu" badala ya "kwa sababu"
- "kwasasa" badala ya "kwa sasa"
- "kwahivyo" badala ya "kwa hivyo"
- "kwakuwa" badala ya "kwa kuwa"
- "kwaniaba" badala ya "kwa niaba"
- "kwaajili" badala ya "kwa ajili"
- "hatahivyo" badala ya "hata hivyo"
- "wapili" badala ya "wa pili"
- "wakwetu" badala ya "wa kwetu"
- "chawenyewe" badala ya "cha wenyewe"
- "yazamani" badala ya "ya zamani"
- "wanavitu" badala ya "wana vitu"
- "elfutatu" badala ya "elfu tatu"
- "miambili" badala ya "mia mbili"
- "mianne" badala ya "mia nne"

Hili ni kosa lililotamalaki katika nyaraka rasmi⁷ nyingi. Inavyoonekana, watu wengi hawajui kwamba kwa kuandika hivyo wanafanya kosa bali wanadhani wapo sahihi. Sababu ya makosa hayo ni kukosekana kwa umakini na kutumia mazoea. Watu wamekuwa wakiambulizana makosa hayo kwa maana kwamba mtu anaposoma waraka rasmi ambao una makosa, anajua hivyo ndivyo inavyotakiwa; hata hivyo, waraka rasmi kutoka taasisi mbalimbali ni rahisi kuaminiwa.

2.2.2 Kutenganisha Maneno Yanayostahili kuwa Neno Moja

Hili ni kosa la kutenganisha neno linalopaswa kuwa neno moja. Kosa hili hufanywa katika maandishi ambapo neno zima linatengwa kwa kuacha nafasi na kufanya yawe kama maneno mawili.

Mfano:

- "aliye nipigia" badala ya "aliyenipigia"
- "alicho kipata" badala ya "alichokipata"
- "atakapo kuja" badala ya "atakapokuja"
- "walimo fikia" badala ya "walimofikia"

⁷ Mifano ya nyaraka haijaoneshwa kwa sababu za kiitikeli.

12 ISSAYA LUPOGO - KUKITHIRI KWA MAKOSA YALIYOZOELEKA KATIKA MATUMIZI YA KISWAHILI SANIFU

“*watakacho kula*” badala ya “*watakachokula*”
“*anacho panda*” badala ya “*anachopanda*”
“*kinacho elezwa*” badala ya “*kinachoelezwa*”
“*walipo chimba kisima*” badala ya “*walipochimba kisima*”
“*mfanya biashara*” badala ya “*mfanyabiashara*”
“*mjasiria mali*” badala ya “*mjasiriamali*”
“*bilashaka*” badala ya “*bila shaka*”

Hili nalo ni kosa lilitotamalaki. Bila shaka watu wanaokosea hudhani kwamba neno kama “asiyependa” linaundwa na maneno mawili: ‘asiye’ na ‘penda’. Huenda wanadhani hivyo kwa sababu neno “asiye” katika baadhi ya miktadha husimama peke yake na kuleta maana. Mfano: “*asiye* na mke hana furaha”. Neno “asiye” linajikamilisha. Tungo nyingine zinazoendana na hiyo ni:

- *Walio* na wake waje hapo
- *Palipo* na wengi hapaharibiki jambo
- *Walimo* wazee ni sehemu nzuri
- *Kijiko* hiki pia baba *anacho*

Ukiangalia tungo hizi, unaona maneno *walio*, *palipo*, *walimo*, na *anacho* yamesimama peke yake na yamejikamilisha katika tungo hizo bila kuunganishwa na maneno mengine. Kwa hiyo, bila shaka hii inaweza kuwa moja ya sababu zinazomfanya mtumiaji wa lugha ya Kiswahili sanifu popote anapoona maneno hayo kudhani kwamba lazima yasimame peke yake. Mtumiaji huyo wa lugha anashindwa kung’amua kwamba “*palipojaa maji*” na “*palipo na maji*” ni miktadha tofauti ya kisarufi/kisintaksia.

2.3 Uchopekaji na Udondoshaji wa Sauti “/h/”

Hili ni kosa lenye sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inahusisha baadhi ya watumiaji wa lugha kuingiza herufi “h” pasipotakiwa katika tungo mbalimbali. Suala hili linaweza kuelezwa kama uchopekaji wa “h” kimakosa. Sehemu ya pili ya kosa hili ni kinyume cha kosa la sehemu ya kwanza ambapo watumiaji wa lugha hudondoshaji hefufi/sauti “h” kimakosa.

2.3.1 Uchopekaji wa “h” Kimakosa

Hili ni kosa linalohusisha kuiambatisha irabu na sauti “h” kimakosa. Kosa hili hufanywa na baadhi ya watu wanaoandika au kutamka “ha” badala ya “a”, “he” badala ya “e”, “hi” badala ya “i”, n.k.

Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya makosa hayo:

"*haya ya kwanza*" badala "aya ya kwanza"
"*hamani*" badala ya "amani"
"*hakidi*" badala ya "akidi"
"*uhimara*" badala ya "uimara"

Katika ufuutiliaji uliofanywa katika vyanzo mbalimbali ili kubainika makosa haya, inaonesha kwamba sehemu hii ya kwanza, watu hawafanyi makosa katika tungo nyingi kama ilivyo katika sehemu ya pili.

2.3.2 Udondoshaji wa Sauti “/h/” Kimakosa

Hii ni sehemu ya pili ya kosa la ukanganyaji wa matumizi ya sauti “h” na irabu. Hili ni kosa linalofanywa na baadhi ya watu kwa kudondosha sauti “h” kimakosa katika maneno yanayopaswa kuwa na sauti hiyo. Ifuatayo ni orodha ya mifano iliyooonekana kukosewa:

“*akuna*” badala ya “*hakuna*”
“*mahali apa*” badala ya “*hapa*”
“*oma*” badala ya “*homa*”
“*ofu*” badala ya “*hofu*”
“*arufu inayonukia vizuri*” badala ya “*harufu inayonukia vizuri*”
“*alisi*” badala ya “*halisi*”
“*ekima*” badala ya “*hekima*”
“*uli chakula*” badala ya “*huli chakula*”
“*aki*” badala ya “*haki*”
“*ereni*” badala ya “*herini*”
“*Kiswaili*” badala ya “*Kiswahili*”
“*aya mambo*” badala ya “*haya mambo*”
“*uyu*” badala ya “*huyu*”
“*nina amu ya kula*” badala ya “*nina hamu ya kula*”
“*uruma*” badala ya “*huruma*”
“*piga odi*” badala ya “*piga hodi*”
“*nitakaa adi kesho*” badala ya “*nitakaa hadi kesho*”
“*maali*” badala ya “*mahali*”
“*njoo hapa araka!*” badala ya “*njoo hapa haraka*”
“*eshima*” badala ya “*heshma*”
“*eko*” badala ya “*heko*”
“*aramu*” badala ya “*haramu*”
“*anaitwa Amisi Abdalah*” badala ya “*anaitwa Hamisi Abdalah*”
“*samaani*” badala ya “*samahani*”
“*udhuria*” badala ya “*hudhuria*”

14 ISSAYA LUPOGO - KUKITHIRI KWA MAKOSA YALIYOZOZELEKA KATIKA MATUMIZI YA KISWAHILI SANIFU

Imebainika kwamba kosa hili hufanyika zaidi katika mazungumzo kuliko katika maandishi, sababu zikiwa ni kukosa umakini katika kuzingatia misingi ya Kiswahili sanifu inayosababishwa na kupuuzia kwa makusudi au kutofahamu.

Aidha, kama ambavyo imeonekana katika mjadala wa makosa ya kukanganya herufi mbalimbali, katika baadhi ya miktadha, kosa hili pia husababisha kubadili maana ya neno na hatimaye kupotosha maana iliyokusudiwa. Mifano wa jozi za maneno yenyе maana tofauti ni:

- araka na haraka
- amu na hamu
- arufu na harufu

Sababu nyingine ya jumla kwa kategoria mbalimbali za makosa yaliyojadiliwa katika makala hii inayowafanya watu kufanya makosa hususani katika maandishi ni kwamba maandiko mengi rasmi yanaandikwa zaidi kwa lugha ya Kiingereza kuliko Kiswahili. Hii inajidhihirisha kutokana na uhalisia kwamba kuanzia elimu ya sekondari hadi ngazi ya chuo kikuu, masomo yote (isipokuwa somo moja tu la Kiswahili) hufundishwa na kuandikwa kwa Kiingereza. Aidha, katika ofisi nyingi za Serikali, lugha inayotumika katika mawasiliano ya maandishi ikiwemo utunzaji wa kumbukumbu katika nyaraka mbalimbali ni Kiingereza. Kwa hiyo, Kiswahili hupata nafasi ndogo sana ya kuandikwa katika miktadha rasmi, suala ambalo linawafanya watu wengi wasijenge umahiri mkubwa katika uandishi kwa lugha ya Kiswahili.

3.0 Mapendekezo na Hitimisho

Makosa yaliyochunguzwa katika makala hii yamekuwa ni kama ya kawaida sana mionganoni mwa watumiaji wa Kiswahili sanifu. Makosa hayo hufanywa katika lugha ya mazungumzo na lugha ya maandishi. Mathalani, kama ilivyoolezwa makosa ya kutumia sauti /g/ badala ya /gh/ huonekana zaidi katika mazungumzo kuliko katika maandishi. Vivyo hivyo, makosa kama ya kutenganisha na kuanganisha maneno kimakosa hujidhihirisha katika maandishi. Pia, imebainika kwamba mwasilishaji wa makala au ripoti fulani anaweza akawa ameandika vema (mf. gharama) katika makala yake, lakini anapoiwasilisha kwa kuongea anatamka/anasema “garama” badala ya “gharama”.

Ili kuepuka makosa haya, makala hii inapendekeza mambo kadhaa ya kufanya kama ifuatavyo:

Jambo la kwanza ni kuendeshwa kwa semina za kurekebisha makosa hayo kwa makundi mbalimbali ya watu mashuhuri na maarufu pamoja na

wanahabari. Watu kama vile wanasiasa, wasanii na wanahabari wanasikilizwa sana na jamii. Kwa hiyo, jamii huiga jinsi wao wanavyoongea au/na kuandika lugha (Kiswahili), na wanaona ndiyo namna sahihi ya matumizi ya Kiswahili sanifu. Watu hao wakipewa semina ya kurekebisha makosa mbalimbali watakuwa mabalozi wazuri kwa jamii katika matumizi mazuri ya Kiswahili sanifu.

Suala la pili, vyombo vyenye dhamana ya kusimamia lugha ya Kiswahili kama BAKITA, BAKIZA, TATAKI⁸, na KAKAMA⁹ visimame kidete kutetea matumizi ya Kiswahili sanifu na kujitahidi kurekebisha makosa mbalimbali yanayofanywa na watumiaji wa Kiswahili katika miktadha rasmi. Hili linaweza kufanya endapo tu vyombo hivyo vitakuwa makini kufuutilia matumizi sahihi ya Kiswahili sanifu katika miktadha mbalimbali rasmi. Vyombo hivyo vivifuatilie pia vyombo vya habari kama vile magazeti, stesheni za televisheni, redio, televisheni za mkondoni, na kurasa za mitando ya kijamii zinazorusha habari mbalimbali; na kuvikosoa vyombo vyote vya habari vinavyobananga Kiswahili sanifu. Inashauriwa hivyo kwa sababu baadhi ya vyombo hivyo vimebainika kuwa na makosa hayo katika baadhi ya habari zake.

Jambo lingine, kwa watu ambao wanakosea kwa kukanganya herufi kama vile kutumia sauti “r” badala ya “l” na kinyume chake, hali inayotokana na athari za lugha mama, watambue suala hilo na kujitahidi kulidhibiti daima. Lupogo & Lupogo (2019) wamebainisha kwamba tatizo ni tatizo kama hujui ni tatizo lakini ukishalijua kuwa ni tatizo si tatizo tena. Hii ina maana kwamba kama unajua sababu za tatizo ni rahisi kukabiliana nalo na hatimaye kulitatua, tofauti na kama hujui sababu za tatizo hilo. Kwa hiyo, watumiaji wa Kiswahili wanapaswa kujua maeneo ambayo wanapata shida katika kuzungumza au/na kuandika Kiswahili sanifu na kuyafanyia kazi kwa maana kuwa na jitihada za kujirekebisha.

Aidha, watumiaji wa lugha wanashauriwa kujenga utamaduni wa kujisomea vitabu na makala zilizotumia Kiswahili sanifu ambazo zimechapishwa na makampuni au majorida ya kuaminika ili kuongeza maarifa hususani kuona jinsi lugha hii inavyoandikwa badala ya kutumia mazoea. Vilevile, wataalamu wa lugha ya Kiswahili wana nafasi kubwa ya kurekebisha makosa yanayofanywa na watu katika majukwaa mbalimbali kama vile katika mitando ya kijamii, katika makongamano na mikutano. Vilevile, watu wanaporekebishwa wakubali kurekebishi. Mwandishi wa makala hii aliwahi kumrekebisha mwanahabari¹⁰ mmoja

⁸ Hii ni akronimu, kirefu chake ni Taasisi ya Taaluma za Kiswahili

⁹ Hii ni akronimu, kirefu chake ni Kamisheni ya Kiswahili Afrika Mashariki

¹⁰ Mwanahabari huyo pamoja na kituo chake hawawezi kutajwa kwa sababu za kiitikeli..

16 ISSAYA LUPOGO - KUKITHIRI KWA MAKOSA YALIYOZOZELEKA KATIKA MATUMIZI YA KISWAHILI SANIFU

kosa fulani, mwanahabari huyo akasema hawezi kurekebisha kwa sababu hivyo ndivyo namna ambavyo kituo chao cha habari kimeamua kutumia lugha ya Kiswahili katika suala hilo. Madai ya mwanahabari huyo si sahihi kwa sababu kama chombo chao cha habari kinatumia Kiswahili sanifu lazima kifuate misingi na kanuni za lugha hiyo ambayo inafanana; na sio kujiundai kanuni tofauti.

Kwa ujumla, lugha ya Kiswahili imechukuliwa kuwa ni lugha isiyotakiwa kutiliwa maanani kama lugha ya Kiingereza. Hii inajidhihirisha wazi pale ambapo mtu akikosea lugha ya Kiingereza lazima atakosolewa na watu wengi sana mitandaoni na katika vyombo vya habari vingine; sote ni mashahidi katika hili. Tumewahi kushuhudia vipande vya video au sauti za watu waliokosea kuongea lugha ya Kiingereza vikizungushwa mitandaoni na katika vyombo vya habari vingine. Lakini hatuoni kamwe hali hiyo ikijitokeza kwa watu wanaokosea Kiswahili. Aidha, baada ya kujaribu kufananisha kiwango cha ufanyaji wa makosa kati ya lugha ya Kiingereza na Kiswahili katika vyombo vya habari vikubwa vinavyotumia lugha hizo mbili katika vipindi tofauti, ilibainika kwamba kiwango cha ufanyaji wa makosa katika Kiswahili ni kikubwa kuliko katika lugha ya Kiingereza.

Huu ni wakati wa Waswahili wote kusimama na kukitetea Kiswahili ili kiandikwe na kusemwa vema. Tunatakiwa kujenga utamaduni wa kukosoana kama ambavyo tu(wa)nafanya katika lugha ya Kiingereza. Tuondoe imani ya kukitazama Kiswahili kama lugha yenyе hadhi ya chini na kukiona Kiingereza kama lugha yenyе hadhi ya juu; tupige vita ubeberu wa kiisimu.

Marejeleo

- BAKITA. (2017). *Mwongozo kwa Waandishi wa Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: BAKITA na TATAKI/TUKI.
- Corder, S. P. (1967). The significance of learners' errors. *International Review of Applied Linguistics*. 9: 161-9.
- Dixon, R. M. W (1997). *The Rise and Fall of Languages*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Ellis, R. (1994). *Second Language Acquisition*. Oxford: Oxford University Press.
- Feltsen, P. (200). Language Acquisition and the Errors We Make: A comparison between beginners and intermediate learners. Mid Sweden University. Inapatikana katika <http://www.diva-portal.org/smash/get/diva2:224418/fulltext01.pdf>.
- Hans, M. (2014). Mchango wa Lahaja katika Kukuza na Kuendeleza Kiswahili Sanifu: Hazina Fiche iliyomo katika Lahaja za

- Kiswahili za Zanzibar. Tasnifu ya Uzamivu. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kiango, J. (2002). Nafasi ya Kiswahili katika ujenzi wa jamii mpya ya Afrika Mashariki. *Swahili Forum*. IX, 143-154.
- Lupogo, I. & Lupogo, A. (2019). *Nadharia ya Utoka kati Ndoa na Mahusiano ya Kimapenzi*. Dar es Salaam: Kiswahili Development Limited.
- Maganga, G. (1991). A Study of the Morphophonology of Standard Kiswahili, Kipemba, Kitumbatu and Kimakunduchi. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- TUKI (2014). *Kamus ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford.
- Whiteley, W. (1974). *Swahili: The Rise of a National Language*. London: Methuen.